YESU alisema: Naja—

upesi

Ufunuo 22:12

Kiziwi na bubu

na Yambaye Guillaume-Yalde, Chad

Nililelewa katika familia ya kikristo na nikaandikishwa katika shule ya msingi katika kijiji changu mwaka 1969. Kwa bahati mbaya mwaka 1976 nilipokuwa kwenye kozi yangu mwaka wa pili nilishikwa na ugonjwa wa uti wa mgongo. Baada ya hapo nikawa bubu na kiziwi, kwa hiyo sikuweza kuendelea na masomo yangu, nikalazimika kurudi kijijini kwangu.

Mwaka 1981 nilijiunga na shule ya Efata ya viziwi wa Chad. Nilisoma pale na kupata cheti changu mwaka 1983. Sikuweza kuendelea zaidi kwa sababu shule za kiziwi huishia shule ya msingi. Kwa hiyo niliamua kwenda N'djamena ambapo nilipokea mwaliko kutoka kwa mkuu wa shule ya viziwi. Nikaanza kozi mpya ya mawasiliano ya viziwi kwa muda wa miaka mitatu, na hatimaye nikapokea cheti cha sifa katika kazi ya useramala. Nikamwomba Mungu mwenye uwezo wote anibariki na kunilinda katika kazi hii.

JE, NIENDE WAPI BAADA YA KUFA?

Kabla sijatoka kijijini, vita vya kikabila vilitokea kwa watu wa makabila tofauti. Watu waliuana kama vile mtu anavyowaua mbwa. Niliogopa kufa kwa vile nilijua ndio ingekuwa mwisho wa maisha yangu hapa duniani na sijui roho yangu ingeenda wapi? Je, nini kitafuata baada ya kufa? Je, inawezekana kuishi tena baada ya kufa? Nafahamu Biblia hueleza juu ya mbinguni na jahanum. Inasema kuwa nitaenda mojawapo ya pahali hapo na yote inategemea hali yangu na uhusiano wangu na Mungu.

Nilipofikiri kuwa kufa ndio mwisho wa maisha yangu Mungu aliniambia, “La, sio mwisho, bado unao muda wa kuishi na unapaswa kutubu na kumwamini Bwana Yesu leo hii, nawe utaokoka. Hii ndiyo saa ya wokovu.” Biblia inasema, **“Amwaminiye Mwana yuna uzima wa milele; asiyemwamini Mwana hataona uzima, bali ghadhabu ya Mungu inamkalia”** (Yohana 3:36).

Niliogopa kupoteza maisha yangu, kwa hiyo niliamua kuyatoa kwa Mungu. Nilitubu kwa machozi na kuomba Mungu anisamehe dhambi zangu zote. Mungu alinisamehe na kunitua mzigo wangu wa dhambi. Hadi sasa Mungu amekuwa mwaminifu kwa ahadi na amri zake. Mungu amenifungulia njia huko Ibadan (Nigeria) kwa ajili ya masomo nami nimepata baraka nyingi za kimwili na kiroho ili niwasaidie ndugu na dada zangu wakristo. Nimepata baraka kwa faraja nyingi na roho yangu imebarikiwa na Neno la Mungu.

Mungu mwenye uwezo

“Mungu kwetu sisi ni kimbilio na nguvu, msaada utakaoonekana tele wakati wa mateso. Kwa hiyo hatutaogopa ijapobadilika nchi, ijapotetemeka milima moyoni mwa bahari. Maji yake yajapovuma na kuumuka, ijapopepesuka milima kwa kiburi chake.”
Zaburi 46:1-3

“Maana milima itaondoka, na vilima vitaondolewa; bali wema wangu hautaondoka kwako, wala agano langu la amani halitaondolewa; asema BWANA akurehemuye.”
Isaya 54:10

“Wewe, BWANA, nguvu zangu, nakupenda sana; BWANA ni jabali langu, na boma langu, na mwokozi wangu, Mungu wangu, mwamba wangu ninayemkimbilia.”
Zaburi 18:1,2

Amekufa

Corbis.com

Na Ezekiel W. Mpapale, Kenya

Mwaka jana tarehe 26 Februari jioni sana nilikuwa nikiendesha pikipiki yangu kwa mwendo kasi sana. Nilijikuta katika lango la kuingilia shule iitwayo Kiunga, katika wilaya niliyokuwa nafanyia kazi kama mwenezaji injili kwa watu wa Boni. Ghafla watoto walitokea katika lile lango. Pikipiki yangu ilikuwa katika mwendo mkali nami nikashindwa kuielekeza. Ilikuwa kwamba ama niokoe maisha ya watoto na mimi nijigonge mtini uliokuwa pembeni au kuendelea moja kwa moja nimwue mmojawapo wa wale watoto.

WALIJUA KUWA NIMEKUFA

Sielewi nini kilitokea kwa sababu nilijikuta nimelazwa katika kituo cha afya kilichoko karibu nikiwa nimeshonwa upande wa kushoto wa uso na damu nyingi ikiwa kila mahali mwilini. Kelele nilizosikia kijijini zilikuwa za kuniogopesha kwani karibu kila mtu alikuwa akisema, “amekufa”. Walijua kuwa nimekufa. Kwa kweli Mungu ni mwema sana kwani baada ya siku chache ndege ilitumwa kutoka Nairobi ambayo ilinipeleka mpaka Hospitali ya Kijabe.

Baada ya miezi kadhaa nilikuwa nimepona, kwa hiyo nilirudi kijijini pale kuonyesha kuwa sikuwa nimekufa kama watu walivyodhani. Nao waliponiona walishangaa sana. Niliwaeleza kuwa Bwana ninayemtumikia ni Mungu wa ajabu ambaye hawezi kuniacha nife kama bado sijamaliza kazi aliyonituma nifanye. Jambo hili liliwasaidia watu wengi sana katika kijiji na wilaya ile wafikiri kuhusu Mungu wa kikristo kwa sababu wengi wao ni waislamu.

Nimepata ushindi

na Don Wilde, Canada

“Don amka! amka!” Hayo ndio maneno ya kwanza niliyosikia nilipozinduka kutoka katika kuzirai. Wauguzi wawili waliosimama pembeni ya kitanda changu wakijitahidi kuniamsha. Nilipofungua macho taratibu, waliniambia ya kuwa nilipata ajali mbaya ya gari. Ajali hiyo ilitokea siku ya pasaka, mwaka 1968.

Nikiangalia na kutafakari maisha yangu naelewa kuwa kama ningekufa siku ile ningeteketea jahanum ya milele. Mungu amekuwa akinitafuta sana; hii ilikuwa ni ajali ya tatu katika maisha yangu. Baada ya kupona ajali hii ya tatu niligundua ya kwamba ilikuwa ni miujiza ya Mungu kuonyesha ya kuwa ananipenda. Nilipoteza fahamu kwa siku tatu hivyo sikumbuki matukio ya ajali niliyopata.

MUNGU ALIJIBU OMBI LANGU

Nilipotafakari baadaye kuhusu hii ajali niligundua kuwa ilikuwa ni jibu la ombi langu kwa Mungu. Nililia kwa kukata tamaa, “Kama kuna Mungu asikiaye maombi, naomba anisikie na anionyeshe upendo wake”. Alifanya hivyo kwa kuokoa maisha yangu. Hatimaye niliyatoa maisha yangu kwa Yesu Kristo. Mungu amenifundisha mengi toka katika maandiko yake, **“Maana nayajua mawazo ninayowawazia ninyi, asema BWANA, ni mawazo ya amani wala si ya mabaya, kuwapa ninyi tumaini siku zenu za mwisho. Nanyi mtaniita, mtakwenda na kuniomba, nami nitawasikiliza. Nanyi mtanitafuta na kuniona, mtakaponitafuta kwa moyo wenu wote”** (Yeremia 29:11-13).

(kwa hisani ya Western Tract Mission, Canada)

✂ Kata hapa

Jina .....No 88/.....

Anwani.....

.....

Nchi .....

UKITAKA KUPOKEA NAKALA YA UPESI BILA MALIPO, andika jina na anwani yako hapa kwa HERUFI KUBWA. Tuma kwa:
UPESI, Box U,
44 Twyford Road
Willington, Derby
England, DE65 6BN
(Ukituma barua bila stampu, au ukitia stampu zisizo mpya, barua haitatufikia.)
Ukitaka kusoma UPESI kwenye INTERNET, tumia: http://soon.org.uk/swahili/swahili.htm

ISSN 1472-7285

Ilinibidi nishinde

na Dominique Azzaro, Tunisia

"Je, anahitaji nini kingine?" watu walikuwa wakiniulizia. Nilikuwa shujaa mpiganaji ndondi wa taifa. Nikawa wakili kwa nchi ya Ufaransa katika michezo ya Olimpiki. Nikawa na marafiki wengi wenye mali walionikaribisha majumbani mwao kwa chakula. Nikakutana na watu wa maana sana. Je, nini kingine nilichohitaji?

Walakini nilisumbuka moyoni. Maisha yangu yalikuwa baridi na matupu. Ndondi zilimiliki kila pande ya maisha yangu na ilibidi nishinde kila mchezo.

Siku moja mke wangu alikaribishwa na rafiki zake kwenda kusikiliza jinsi ya kutosheka katika maisha. Akaenda nao, naye akawasikiliza wakiongea habari za Yesu. Amelisikia hili jina awali lakini hakujua chochote kuhusu Yesu.

Baadaye aliniambia, "Yale waliyozungumza kuhusu Yesu yalileta maana kwangu. Watu wote katika mkutano waligundua njia ya kuridhika katika maisha yao. Ndipo niliamua kuongea na Mungu kuhusu maisha yangu katika huo mkutano, na sasa Mungu amenibadilisha! Sasa nimejawa na furaha."

NILISHINDWA PAMBANO LA NDONDI

Usiku uliofuata nilishindwa pambano la ndondi, nikahuzunika sana. Mke wangu alizidi kunisisitiza ili nimwombe Mungu anibadilishe maisha yangu kusudi nione raha. Siku moja niliamua kwenda naye katika mkutano nipate kusikiliza hawa rafiki zake wapya wanasema nini. Katika ule mkutano nilitambua ghafla kwamba kupiga watu kwenye shindano la ndondi hakunipa furaha ambayo watu waliokuwa mkutanoni wameipata.

Nilipowauliza kwa nini wako tofauti walinielezea kwamba Yesu amewasamehe makosa yao na dhambi zao. Wameisha kugundua furaha ya kweli katika kumtumikia. Ndipo nilipoamua kumwomba Yesu anisamehe dhambi zangu na yale yote mabaya niliyoyatenda. Maisha yangu yamebadilika.

Watu wakaanza kusema kwamba Dominique yuko tofauti, wengine wakasema nimekuwa kichaa! Ya kuwa ubongo wangu umeharibika kutokana na machezo ya ndondi!

Sikuwajali yote waliyosema kuhusu mimi. Sasa hivi nimepata furaha ya kweli. Hata wewe, unaweza kupata hii furaha hali kadhalika.

Nilikuwa na wasiwasi

na Kambale Kitsongo, D.R. Congo

Mimi ni kijana wa umri wa miaka 17 nikazaliwa katika familia ya kikristo ambao wazazi wangu walimtumikia Mungu. Tangu utoto wangu sikuiba wala kudanganya wala kusema maneno ya kuumiza. Pia nikaamini kwamba nitaenda mbinguni, mimi na wazazi wangu. Sikufahamu ya kwamba Biblia inasema, **"Maana kila mtu atalichukua furushi lake mwenyewe"** (Wagalatia 6:5).

Nilipokuwa mkubwa, dini ilikuwa ni mzigo kwangu kwani ilinizuia nisitembee ovyo pamoja na wasichana na vijana wengine wa umri wangu. Kwa hiyo nilianza kuishi kama rafiki zangu. Nilifuata jinsi walivyoishi walakini nikiwa pamoja na wakristo wenzangu nilijaribu kubadilika. Niliwategemea sana watu wengine. Nami nilikuwa na wasiwasi sana.

Lakini kwa neema yake Bwana Yesu Kristo aliniita na kunifunulia siri yake. **"Si kila mtu aniambiaye Bwana, Bwana, atakayeingia katika ufalme wa mbinguni; bali ni yeye afanyaye mapenzi ya Baba yangu aliye mbinguni"** (Mathayo 7:21). Aliniokoa akaahidi kunitunza siku zote. Tangu siku ile rafiki zangu wamenidharau kwa sababu ya kumfuata Yesu Kristo, Mwokozi na Mfariji wangu.

Natembea tena!

Na Mwemema Kana-Kamo, Zambia

Mimi nilizaliwa mwaka 1957. Nilipotimiza miaka 15, nilishikwa ugonjwa ambao ulipoozesha miguu yangu. Nilisumbuka sana hadi umri wa miaka 20 kwa sababu sikuweza kutembea wala kuketi. Siku hizi zote nilikuwa hospitalini. Madaktari hawakuweza kunitibu. Nilichukuliwa kwa waganga wa kienyeji walionipa madawa mbalimbali walakini sikupona. Hatimaye, wanilipeleka nyumbani mwa wazazi wangu.

NILISHTUKA KATI YA USINGIZI

Usiku mmoja niliota ndoto. Mtu mmoja mwenye mavazi meupe sana alinijia na kunigusa akisema, "Inuka, utembee." Nilishtuka kati ya usingizi nikatambua kuwa sikuwa na maumivu tena miguuni.

Asubuhi yake nilitembea. Kila mtu alishikwa na mshangao mkubwa aliponiona nikitembea. Mpaka leo ningali mzima. Yesu aliniponya. Aliweza kufanya ambavyo madaktari na wachawi walivyoshindwa kufanya. Ndugu zangu, acheni kupoteza muda kwa kuwaendea wachawi. Mtumainiye Yesu mwenye uwezo wote.

Sikiliza Redio!

Kupokea Habari Njema katika lugha ya Kiswahili kwenye **Redio FEBA** kwa **Redio Habari Maalum** sikiliza 11885 kHz, Mitabendi 25 kila siku:
Asubuhi: Saa 12 na robo;
Usiku: Saa 1 na robo.
TWR: 5970 kHz, MB 49: Saa 12 kila asubuhi; 9440kHz, MB 31: Saa 2 kila usiku.
Mombasa-**Baraka FM** - Kwenye 95.5FM katika Kiswahili na Kiingereza.

Mchele, mayai au kahawa?

Kijana mmoja alilalamika kwa baba yake kuwa maisha yake yalikuwa magumu sana. Kazi yake ilikuwa siyo nzuri, mke wake alikuwa siye mzuri, kodi zilikuwa ghali kupita kiasi na serikali nayo ilikuwa mbaya.

Babake alimpeleka jikoni. Akajaza maji katika sufuria tatu na kuziweka jikoni. Maji yalipoanza kuchemka baba alitia mchele katika sufuria moja, mayai kwenye sufuria nyingine na kahawa iliyosagwa kwenye sufuria ya tatu. Aliacha zichemke na kisha akaziondoa kwenye moto ili zipoe pamoja na vilivyoko ndani.

Baada ya muda mrefu alimgeukia mwanawe na kumwuliza, "Unaona nini katika sufuria hizo?" Kijana alimjibu, "Ninaona wali, mayai na kahawa." Baba alimpa kijana vijiko vitatu vikubwa ili achote kiasi kidogo kutoka kwenye kila sufuria. Baada ya kuchota, kijana hakuweza kujua babake alikuwa akimfundisha nini, kwa hiyo aliuliza, "Baba, hiyo ina maana gani sasa?"

MATOKEO TOFAUTI

Kwa upole baba yake alianza kumweleza kuwa kila kitu katika zile sufuria kilipata moto wa mateso sawasawa lakini matokeo yake yalikuwa kabisa tofauti: mchele ulilainika sana, mayai yalikuwa magumu kama mwamba lakini kahawa iliyabadilisha maji na kuyafanya yawe na harufu nzuri na ladha ya kupendeza. Hivyo akasema, "Mwanangu, sisi pia tunaweza kuyafanya matatizo yetu yatufanye magumu ndani yetu, kama yale mayai ambayo yalipikwa kwa muda mrefu. Au pia tunaweza kuyaruhusu yatuvuruge mawazo na roho zetu kama ule mchele uliopikwa sana na kuvurugika.

"Lakini pia tunaweza kumgeukia Yesu kumwomba atubadilishe na kutufanya kama ile kahawa iliyoyafanya yale maji yakawa mazuri. Ni Yesu peke yake anayeweza kutubadilisha lakini ni lazima yetu tumruhusu. Ukifanya hivyo maisha yako yatabadilika yawe mazuri zaidi."

Jifunze kitabu cha Mungu

Ukitaka kupata Masomo ya Biblia katika lugha ya Kiswahili kwa posta, tuma jina na anwani yako kwa:
Katika KENYA: Emmaus Shule ya Biblia, SLP 72725, Nairobi, Kenya.
Katika CONGO: Cours Biblique Emmaus, BP 350 Bunia, Rég. du Haut-Congo, Rép. Dém. du Congo.
Katika TANZANIA: Emmaus Shule ya Biblia, SLP 1424 Dodoma, Tanzania. Wanasubiri barua yako ili uweze kutumiwa somo lako la kwanza bila malipo.